

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Usalama wa Raia ni Kadhiya Muhimu Mno na Haipaswi Kuchukuliwa kwa Usahali

Kifo cha mwanafunzi mmoja na kujeruhija vibaya kwa wanafunzi thelathini wa Chuo Kikuu cha Strathmore katika jiji kuu la Nairobi katika Zoezi lililo kwenda mrama la Kupambana na Ugaidi ni jambo la kuvunja moyo na ambalo lastahili kukemewa na kila muekaji amani. Ripoti kutoka kwa vyombo vya habari nchini zimesema kuwa tukio hilo lilipangwa na uongozi mkuu wa Chuo hicho kwa ushauriano na maafisa wakuu wa polisi bila ya kuwaarifu wanafunzi hao.

Ruhusa iliyotolewa kwa kitendo hicho kiovu cha kigaidi imethibitisha namna vyombo vya usalama vinavyo vuruga na kuhatarisha usalama wa raia. Kwa nini vitendo kama hivyo vyenye kupelekeea kupoteza maisha na majeraha kwa watu vivumiliwe kufanyika kwa kisingizio cha matayarisho dhidi ya mashambulizi ya kigaidi! Ni vipi inaingia akilini kwa upande mmoja kudai kupigana na ugaidi huku upande mwingine ukitekeleza vitendo vya kigaidi vinavyo pelekea majeraha na kupoteza maisha? Hili haliwezi kushabikiwa ikizingatiwa kuwa kadhiya ya usalama ni maslahi muhimu mno kwa watu na ambayo serikali na taasisi zake ina jukumu la kulinda raia wake. Tumeshtushwa na wanaodaiwa kuwa wasomi na ambao pia ni wasimamizi wa chuo hicho kuwaona wakichukua maisha ya watu kwa urahisi ambapo hata wajinga wa mwisho kabisa huyatukuza na kuchukua tahadhari kuyalinda.

Bado tungali tunaiona Kenya ikiendelea kupalilia njama ya dola za Kimaghribi hususan Amerika kuuhusisha Uislamu kimakusudi na vitendo vya kigaidi. Dola hizo zimekuwa zikiwatoa sadaka raia wake ili kuwalazimisha waziunge mkono katika mauaji yao ya kinyama ya Waislamu. Tunahisi kitendo hiki kililengwa kulazimisha fikra kwa wasiokuwa Waislamu za kuendelea kuwachukia Waislamu na kuwaona kama tishio kwa usalama wa watu wote wakiwemo wanafunzi.

Uislamu unatambua kuwa kadhiya ya usalama sio kadhiya inayopaswa kuchukuliwa kwa usahali na ndio sababu ukailazimisha Dola ya Kiislamu, Khilafah, kudhamini usalama kwa wanadamu. Kulinda maisha ya mwanadamu ni moja ya mafunzo ya Uislamu. Sheria imeeleza ndani ya Qur'an:

مَنْ أَجْلَ ذَلِكَ كَتَبْنَا عَلَى بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَلَّمَنَا قَتْلَ النَّاسِ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَلَّمَنَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا

"Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliye muua mtu bila ya yeye kuua, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote." [TMQ Al-Maidah: 32]

Shabani Mwalimu

Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Afrika Mashariki